# Tutaendelea kuilinda misitu ya hifadhi – Shamata

NA SALAMA MOHAMMED, WKUMM

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema serikali itaendelea kuimarisha ulinzi katika misitu ya hifadhi ili isipoteze uhalisia hatua ambayo itaongeza kasi ya maendeleo ya sekta za kilimo na utalii.

Shamata alieleza hayo wakati wa ugawaji wa sare za kazi kwa wafanyakazi wa kitengo cha uhifadhi wa msitu wa Kiwengwa Pongwe, wilaya wa Kaskazini 'B', mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema hatua hiyo inalenga kuimarisha mashirikiano kati ya wizara hiyo na Mwekezaji kutoka katika kampuni ya Michel Mantheakis Safari Zanzibar Ltd katika kutekeleza shughuli mbali mbali za ulinzi na uendelezaji wa msitu huo.

Waziri huyo aliwasisitiza wafanyakazi hao kuvaa sare hizo wanapokuwa kazini ili kuwarahisishia wananchi na watalii wanaotembelea eneo hilo kuwatofautisha na watembezaji wageni, ili kuimarisha ulinzi katika maeneo ya hifadhi.

Aidha, alisema serikali haitosita kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaofanya uharibifu wa msitu huo kwa kufanya shughuli mbali mbali zinazopelekea kutoweka kwa maliasili zinazopatikana ndani ya msitu huo.

Aliongeza kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la uvamizi wa msitu huo kwa shughuli za kibinadamu zikiwemo za kilimo, ujenzi, ukataji wa miti kiholela na uchomaji moto katika hifadhi ya msitu, mambo ambayo yatapelekea kupoteza haiba na uhalisia wa mazingira iwapo uhifadhi mzuri na ulinzi utakosekana .

"Serikali yetu inategemea rasilimali misitu kwa sababu ikitunzwa vizuri itapelekea kupatikana kwa mazingira mazuri, hewa safi, maji safi, kuongezeka kwa idadi ya watalii na uwiano wa viumbe hai, hivyo ni wajibu wetu kutunza hifadhi zetu ili tuweze kukusanya mapato kwa ajili yetu na taifa kwa ujumla", alifafanua Shamata.

Kwa upande wake Meneja wa Mradi wa uhifadhi wa msitu huo Said Hassan Mnkeni, amesema lengo la mradi huo ni kuanzisha uwindaji wa kitalii wa paa nunga ili kuongeza idadi ya paa katika hifadhi na kuinua pato la Serikali.

Said aliwasisitiza, wafanyakazi wa msitu huo kushirikiana na jamii inayozunguka msitu huo kwa kuwapatia elimu ili waachane na tabia ya uharibifu wa mazingira.

Kwa upande wake Naibu Sheha wa Kiwengwa Pongwe, Vuai Ame Kombo, alisema watahakikisha jamii inazingatia uhifadhi wa rasilimali za msitu huo ili zibaki salama na kuacha kufanya uvamizi na uharibifu wa maliasili zinazopatikana ndani yake.

Aidha aliisihi jamii kuacha kuharibu maliasili zilizowazunguka kwani msitu huo ni canzo muhimu cha kuinua uchumi na taifa pamoja na upatikanaji wa ajira.

Mapema Msaidizi Mkuu wa hifadhi hiyo, Mohamed Kombo Khatib, akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wenziwe ameeleza kufurahishwa kwao kutokana na kupatiwa sare hizo kwani zitawasaidia kuimarisha ulinzi na kuaminika kwa wanajamii wanaoizunguka hifadhi ya msitu huo.

Msitu wa Kiwengwa Pongwe una ukubwa wa kilomita za mraba 33 sawa na hekta 3,332 na umezungukwa na vijiji 13 ukiwa na jumla ya wafanyakazi 20 waliopatiwa sare hizo zilizogharimu shilingi milioni 4.2.

## Aliyemjeruhi mke mwezake kufikishwa mahakamani leo

NA KHAMISUU ABDALLAH

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, leo linatarajia kumfikisha mahakamani, mtuhukiwa Khadija Shaaban Ali (34) mkaazi wa Chukwani kwa tuhuma za kumjeruhi mke mwenzake kwa kisu sehemu mbalimbali za mwili.Akitoa taarifa kwa vyombo vya Habari, Kamanda wa Polisi mkoa wa Mjini Magharibi, SACP Richard Thadei Mchomvu, alisema bado wanamshikilia mwanadada huyo anayetuhumiwa kufanya tukio hilo na kumuhoji na kubaini kuwa tukio hilo limechochowa na wivu wa mapenzi.

Akizungumzia mume wa wanandoa hao, alisema ndie aliyetoa msaada kufanikisha mke wake kufikishwa polisi bila ya kukimbia na kumtaja mtuhumiwa huyo kuwa ni Khadija Shaaban Ali (34) makaazi wa Chukwani.

"Katika tukio hilo Maimuna Said Suleiman (38) alijeruhiwa kwa kukatwa kwa visu maeneo mbali mbali ya mwili wake na mke mwenzake aliyetambulika kwa jina la Khadija Shaaban Ali (34) wakaazi wa Chukwani mnamo Febuari 9, mwaka huu majira ya saa 7 za mchana", alieleza SACP Mchomvu.

Alibainisha siku ya tukio wote watatu walikuwepo pamoja wakiwa kwenye gari na walipofika nyumbani kwa mke mdogo ghafla mke mkubwa anatoka kwenye gari alitoa kisu kuanza kumshambulia mke mdogo wakati mume wao akiwa ameshaingia ndani ya nyumba

Alisema majeruhi huyo anendelea kupatiwa na matibabu katika hospitali ya Mkoa Lumumba na hali yake inaendelea vizuri hivyo alitoa wito kwa jamii kutochukua sheria mikononi wanapokuwa na chuki au sababu yeyote badala yake watumie njia sahihi kusuluhisha ikiwemo ya kuwashirikisha wazee na wazazi waliosimamia ndoa zao kuwapa ushauri na kukaa kwa amani.

"Sio kitu cha ajabu kuwa na wanawake wawili au zaidi bali inapotokea kutofautiana kwa kuhisi kwamba yeye anapendelewa sio busara kumshambulia kwani unaweza kujitafutia matatizo zaidi, ukiwa mke mwenza uwe mtulivu maisha yaende na kuishi kwa busara", alisema Kamanda Mchomvu.

Akizungumzia hali ya ulinzi na usalama katika mkoa huo, Kamanda Mchomvu alieleza kuwa imeendelea kuimarika na mkoa upo salama na wananchi wanaendelea kufanya shughuli zao kwa amani na utulivu.

"Yapo matukio ya kihalifu yaliyojitokeza Febuari 5 na 6, mwaka huu katika maeneo ya Sogea na Magogoni ambako kulijitokeza tukio la vijana watano kuvamia nyumba tatu na kufungua milango kwa nguvu, kujeruhi watu na kuiba simu", aliongeza.

Alisema matukio hayo yalileta sura mbaya kwa jamii na kuingiwa na hofu hivyo aliwahakikishia wananchi kuwa Jeshi la Polisi litaendelea kuwalinda raia na mali zao ili wishi kwa amani na utulivu na kufanya shughuli zao za kujiletea maendeleo na kwamba matukio ya kihalifu yanayashughulikiaw na tayari mtu mmoja amekamatwa akihusishwa na tukio hilo.

.

Mbali ha hayo aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na jeshi hilo kwa kutoa taarifa watakapobaini matukio ya uvunjifu wa amani ili wahalifu waweze kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.



WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mahmoud Thabit Kombo (katikati), akiwasili jijini Addis Ababa, Ethiopia kwa ajili ya kikao cha 46 cha Baraza la Mawaziri la Umoja wa Afrika (AU) kilichoanza jana. (PICHA NA WMNUAM).

## Mapokezi makubwa yamsubiri Dk. Mwinyi Pemba

NA BAKAR MUSSA, PEMBA

KATIBU wa Idara ya Siasa, Itikadi na Mafunzo wa Chama cha Mapinduzi Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis, amewataka wana-CCM na wananchi kujitokeza kwa wingi kwenye mapokezi ya mgombea wa Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anaetarajiwa kuwasili kisiwani humo Februari 15 mwaka huu.

Mbeto alieleza hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za CCM mkoa wa Kusini Pemba.

Amesema mgombea huyo ambae atawasili kisiwani humo mara ya kwanza tangu kumalizika kwa mkutano mkuu maalum wa CCM uliomuidhinisha kuwa mgombea wa urais kwa tiketi ya CCM, atapokewa na wana-CCM na wananchi.

Mbeto alisema akiwa kisiwani Pemba, Dk. Hussein atapa fursa ya kuonana na wazee wa CCM katika ukumbi wa Manispaa ya mji wa Chake Chake na baadae atazungumza na wananchi wa mikoa miwili ya Pemba.

"Mapokezi yalifanyika Unguja baada ya kumalizika mkutano mkuu wa Dodoma na kama kawaida Mgombea huyo mteule atapatiwa mapokezi Kisiwani Pemba kama yaliofanyika kule Unguja", alisema.

Aliwataka wana CCM pamoja na wananchi kujitokeza kwa wingi katika mapokezi yatakayoambatana na mkutano huo ili kuunga mkono maazimio ya mkutano mkuu wa CCM Taifa juu ya azimio hilo na kumuunga mkono Dk. Hussein Ali Mwinyi kutokana na juhudi zake za kuleta maendeleo nchini.

Akizungumzia zoezi la uandikishaji wa daftari la kudumu la wapiga kura Kisiwani Pemba, Mbeto aliwapongeza wananchi kwa kujitokeza kwa wingi katika uandikishaji wa awamu ya mwisho ya daftari la wapiga kura ili kuhakikisha kila mmoja anapata haki ya kupiga kura.

Aliwataka wananchi katika Wilaya ya Mkoani kuitumia fursa hiyo ili waweze kupata haki yao ya msingi na kushiriki katika uchaguzi mkuu ujao huku akiwataka wananchi katika Wilaya za Unguja kujiandaa kujitokeza kwa wingi katika uandikishaji huo muda utakapo wadia.

Mbeto, aliwasihi wananchi ambao wamejiandikisha kutunza shahada zao kwani ndio silaha pekee itayoamuwa kuchagua kiongozi wanayemtaka pindipo wakiingia katika chumba cha kupigia kura.

Aidha aliipongeza Tume ya Uchaguzi Zanzibar ((ZEC) kwa juhudi wanazichukuwa katika kuhakikisha kila raia mwenye sifa ya kuandikishwa anapata haki sambamba na kuondoa kasoro ndogo ili wananchi wapate haki yao ya kidemokrasia.

Aliwataka wanasiasa kutotengeneza mambo yasiokuwepo kwenye zoezi hilo kwa kutafuta umaarufu wa kisiasa na kuwatia hofu wananchi, kwani zoezi hilo limekwenda vizuri na ni imani ya CCM wananchi wanayo dhamira njema ya kuchaguwa maendeleo.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na kudumisha amani, umoja na utulivu uliopo nchini ili kuwafanya viongozi waweze kuleta maendeleo yao kwani kila sehemu ya kisiwa cha Pemba imebadilika sasa.